# KARIBU KATIKA KANISA LA MUNGU LA KIMATAIFA

**Iwapo umejifunza kutuhusu kupitia familia yako na marafiki, tovuti ya kiulimwengu, au ratiba yetu kila juma kwenye runinga, Armor of God (Ngao ya Mungu), tunafurahia kuweza kuwasilisha ujumbe ufuatao kuhusu kanisa letu na mafunzo zetu. Tunawakaribisha katika "nyumba" yetu na ushirika.**

**Kijitabu hiki kimeandikwa kukueleza kuhusu Kanisa la Mungu la Kimataifa na shughuli zake. Hatujajaribu kueleza kila kitu kwa undani hapa. Tuko na fasihi na habari ambazo zinaweza kujaza mwanya. Kama unao swali lolote, usikose kutuandikia ama kutupigia.**

## Mbona uwe na Kanisa?

Biblia ni rekodi ya historia ya Mungu na uhusiano wake na viumbe vyake. Alimweka mwanadamu hapa duniani kwa kusudi fulani maalum; kusudi ambalo linafunua mpango waka kwa kila mwanaume, mwanamke na mtoto ambaye ameweza kuishi.

Kutokea mwanzo, Mungu alimpa mwanadamu mwongozo. Aliwasilisha mapenzi Yake kwa viongozi, waamuzi kisha kwa manabii. Mwishowe, Mwana wa Mungu Yesu Kristo, alikuja hapa duniani kama "mjumbe." Yesu alifunua kusudi sawa iliyowasilishwa kupitia miaka.

Waebrania 1:1-2 inatuambia, *"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu mingi na kwa njia mingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika mwana…"*

Kupitia injili tunajifunza kwamba Yesu alianzisha kanisa. Alikuwa jiwe la msingi (Waefeso 2:20) ambalo waumini ililipaswa au linapaswa kuanzika. Ili kumsaidia kuhudumia ubinadamu na kuwasilisha ujumbe wake, Yesu alwachagua wafuasi kumi na wawili. Aliwafundisha kuwa msingi wa kanisa lake. Akijua hatakuwa nao kimwili zaidi ya mafunzo yao kwa miaka mitatu na nusu, waliahidiwa uwepo wake kupitia njia nyingine. Aliwaambia, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu

yenu roho mtakatifu” (Matendo 1:4-8). Siku ya Pentekoste (Matendo 2) wafuasi, jinsi ilivyoahidiwa na Yesu, walipokea nguvu isiyo ya kawaida ya Roho Mtakatifu.

Kufuatia maonyesho ya Roho Mtakatifu wanafunzi walieneza ujumbe wa Kristo ulimwenguni. Wengi waliosikia walijiunga pamoja kwa ibada. Waliobadilika hawa waliunda kundi lililojulikana kama kanisa (Kigiriki = ecclesia) au “wenye mwito.” Kile kilichoanzishwa karibu miaka elfu mbili zilizopita kinaendelea hadi sasa. Watu kama hao bada wanaabudu pamoja, wakihubiri na kueneza injili.

Wanafunzi waliambiwa na Yesu *“kufunza mataifa yote, wakiwabatiza…na kuyashika yote niliyowaamuru…”* (Mathayo 28:19-20). Wakiwajibika kwa amri hii ya “ufunzi,” Kanisa la Mungu la Kimataifa wako na upande wa misheni wake ya kuwatafuta wapotevu wa kiroho (Luka 19:10). Pamoja na hii misheni, kuna pia upendeleo wa “kuwalisha kondoo” na kuwachunga wakristo jinsi mchungaji huchunga kondoo (1 Petro 5:2). Kanisa la Mungu la Kimataifa linahudumia kama rasilimali kwa kusudi hizo.

Leo, maelfu ya familia wanakuja kwa Kanisa la Mungu la Kimataifa ili kuelewa biblia, amri, elimu na mafunzo. Mahitaji zao zinahudumiwa kupita huduma, ushirika, vipindi vya Ngao ya Mungu, CD/DVD, mahubiri, fasihi bila malipo ikiwemo masomi ya mafundisho ya kibiblia, na gazeti kwenye tovuti kwa watu wachanga (INFUSE Magazine), na habari ya kimataifa, linalosaidia kwa makutano ya kawaida.

Ushirika kwa Kanisa la Mungu la Kimataifa linajumuisha wale “wenye wito” kutoka kote ulimwenguni wanaojifunza ukristo jinsi ilivyoanzishwa na Kristo na kuendelezwa na mitume wa kwanza. Kanisa lilianzishwa na Yesu, vile aliahidi itaendelea kupitia karne, bado ipo hadi sasa. Leo, katika karne hii ya ishirini, kuna wanafunzi wanaoendelea katika imani “waliokabidhiwa watakatifu” (Yuda 3). Walitii ujumbe sawa iliyofundishwa na Yesu Kristo, injili sawa ikienezwa ulimwenguni na wanafunzi. Washirika wanahifadhi ushahidi na mafunzo za Yesu Kristo kama kazi ya kanisa.

## Kanisa la Mungu la Kimataifa linaanzishwa

Julai 1978 Kanisa la Mungu la Kimataifa ilianzika Texas. Ofisi ilianzishwa mashariki mwa Texas, katika jamii ya Tyler. Mwanzoni, barua zilitumwa kwa nyumba za kibinafsi na ombi za habari zikiwasilishwa kwa simu. Kufuatia mwanzo huu, ilikuwa muda mfupi hadi kanisa likapata vifaa za kueneza na kuhudumia washirika ulimwenguni kote. Hadi leo mwanzo wa kimwili inamilikiwa na washirika wa kanisa kwa wingi, na haimilikiwi na mtu binafsi au familia.

Ili kuhudumia washirika kuwasilisha uenezaji, kanisa limeapisha huduma. Huduma hii linatumika kama "wasaidizi wa furaha ya watu" badala ya huduma ya umilikaji (2 Wakorintho 1:24). Wajibu wa kifedha na matumizi inashughulikiwa na Bodi ya wakurugenzi na mamabo ya kikanisa yanaangaliwa na baraza la mawaziri.

## Huduma za Kanisa

Tofauti na makanisa makubwa, Kanisa la Mungu la Kimataifa ni ndogo lakini imetawanyika. Katika kiwango cha mtaani, kinaweza sababisha ibada iliyo tofauti kutoka kwa kile ambacho umewahi kupitia. Hata hivyo, wengi wanapata burudisho zaidi ya makanisa za kinyumbani yaliyotajwa katika agano jipya. Chache za kusanyika zetu wanao jumba lao wenyewe, lakini wengine wanakutana kwenye maboma na mengi katika vyumba vya kukodesha au kwenye ukumbi. Uzuri wa idadi hizi ndogo za kusanyiko ni mazingira ya kifamilia na uwezekano wa kanisa linalojali. Mengi ya kanisa hizi ndogo (saa zingine vinaitwa vikundi vya ushirika) wanapokea kanda za mahubiri kwa wale waliotambuliwa na Kanisa. Hata kama wanao mtumishi, kusanyiko mingi wanaonelea kutazama hizi rekodi za mahubiri. Hii inawapa tangazo za kisasa na uhusiano kwa kazi zaidi ya hiyo kutimizwa mtaani.

Kwa wale washirika ambao kwa sababu ya umbali au hali hawawezi kufika kwa ushirika, tunatoa huduma iitwayo Huduma ya Kanisa iliyopanuliwa. Ikipatikana kwa ombi, mahubiri zinapatikana kila wiki na zinatumwa kwa wakristo waliotawanyika. Huduma ya Kanisa iliyopanuliwa haipaswi kuchukua mahali pa ushirika wa kimtaani. Imeundwa kwa wale ambao kwa njia fulani hawawezi

kufikia kusanyiko la waaminio. Watu wengi wanatumia huduma hii, wengine wakiwasilisha familia na marafiki na wengine kivyao.

Kanisa zinapoendelea, kwa umuhimu zinakuwa na muundo isiyo ya rasmi. Kikundi kinapokuwa kikubwa na kufikia matarajio wanafanya ombi la mkataba. Mahitaji ya kutambuliwa kama ushirika au kikundi cha Kanisa la Mungu la Kimataifa yamewekwa kwa Mwongozo kwa Makanisa, yaliyomo kutoka ofisi yetu kupitia ombi.

## Muundo wa ibada

Huduma za ibada za Kanisa la Mungu la Kimataifa huwa na nyimbo chache na kufunguliwa na maombi, mahubiri (ujumbe wa dakika 10 – 15) au muziki maalum, tangazo, mahubiri (wa dakika 45 au saa moja), halafu nyimbo ya mwisho na maombi. Hakuna mwito wa madhabahu au sadaka inayochukuliwa wakati wa ibada ya kila wiki. Ikiwa unatoka kwa kanisa iliyo na kiwango cha juu cha ibada, utapata Kanisa la Mungu la Kimataifa wa kuburudisha zaidi, wenye mpango mzuri, na inayokaribisha.

Mafunzo za kibiblia na mahuburi ni muhimu kwa ukomavu wa kikristo na ni kuu katika ibada zetu. Tunahimiza wakristo wetu kuchukua jukumu kuhudhuria kila sabato.

Katika Muundo wa 1 Wakorintho 14, liturujia ya kikanisa yapaswa kuinua, wenye mpango, na iliyopangika. Kama Mtume Paulo alivyoandika, *"Basi, ndugu, imekuwaje? Mkutanapo pamoja, kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga."*

## Mavazi Sahihi

Wengine wameuliza kuhusu mavazi sahihi kwa ibada za kanisa. Swali hii kwa ujumla unazingatia ikiwa mavazi rasmi yanahimizwa.

Kanisa la Mungu la Kimataifa hailazimishi aina fulani ya mavazi ili kuja kwa ibada. Tunapendekeza kuwa kile kinachovaliwa kikuwe safi, na pia rasmi. Wadogo

na wakubwa wakikusanyika pamoja, aina mbali mbali inatarajiwa kuhimiza. Kulingana na kule unakoishi, aina mbali mbali za nguo inamuliwa kwa kitamaduni au sherehe spesheli. Hali yoyote ile, jinsi unavyojivaa bila shaka inaonyesha kunamfurahisha Mungu na inaonyesha ule mwanga unaotoa kwa ushirika.

Kanisa mingi za kifamilia wanahudhuria ibada wakivaa kile kwa utamaduni inajulikana kama “nguo za kanisa”- suti na tai kwa wanaume na rinda kwa wanawake. Wengine, pengine wakisawishiwa na konda la kisasa, wanapendelea mavazi kawaida.

Mara kwa mara wengine wanajali ikiwa nguo zao ni bora au sio bora zaidi kwa kuenda kanisa. Ingawa hoja hiyo inafahamiwa, ni muhimu kwenda kanisani kwa kile unacho badala ya kukosa kwenda kamwe. Nguo yoyote ni mzuri kama ni safi. Mungu atafurahia ikiwa umevaa kile unacho upoabudu jinsi uwezavyo.

## Siku ya Sabato

Wakati mwingine, maisha inaweza kuhisi kama mbio za kipanya kwa kila saa ukiamuka kwa shughuli kutoka kwa kazi ya kimapato na kazi za kinyumbani. Wengine watafurahia kuwa huru kwa siku moja bila ya kazi.

Majukumu za dunia hii inamfanya mtu kuwa na wakati mgumu sana wa kumpa Mungu nafasi, familia, na kwa wengine, na hata mambi na masomi ya kibiblia. Lakini Mungu, katika hekima yake ametupatia siku moja kwa wiki kufanya mambo kama hayo. Ilitengenezewa kwa mwanadamu (Marko 2:27) kama siku moja kwa wiki kuwa huru kwa kazi. Hata hivyo tunamkumbuka Mungu na kutafakari juu yake kila siku, siku hii moja imewekwa kando kwa kumwabudu.

Kanisa la Mungu la Kimataifa linatazama jumamosi kama siku ya sabato badala ya jumapili. Kuna siku saba kwa wiki za kalenda. Wiki huanza kwa jumapili (siku ya kwanza) na inaisha jumamosi (siku ya saba). Siku huanza jioni na kumalizika keshoye jioni. Ikiwa maarifa hii inatumika kwa kalenda yetu, tunaona kwamba sabato hakika huanzika siku ya ijumaa jioni na kuisha jumamosi jioni. Ikiwa unataka kujua wakati jioni huanzika kwa siku, unaweza kutazama gazeti yako upande wa hali ya hewa au nenda kwenye mtandao mahali habari hizo

zinapatikana. Iweke kama mazoea kujua wakati sabato huanza ili kumaliza kazi zako.

Kwa sababu Mungu anaamuru kuwa kazi zote zinapaswa kufanywa kwa siku sita na sabato ni siku ya mapumziko, matayarisho yanafaa kufanywa siku ya ijumaa ili kuwe na uwezekano. Tamaduni ya ijumaa kama "siku ya matayarisho" inaturudisha kwa Kutoka 16. Mafundisho mawili yanatokea kwa sura hii. Moja, Sabato sio tu siku moja kwa saba, lakini siku ambayo imeundwa na Mungu. Pili, siku kabla ya sabato ni siku ya kujitayirisha kwa ajili ya sabato.

Vitu vingi vinaweza kufanywa siku ya ijumaa ili sabato iweze kufurahisha. Jaribu kutengeneza boma yako (kupika na kufanya usafi) ili siku ya mapumziko isiwe kama siku nyingine. Maendeleo za kisasa zinarahisisha kupika vyakula mapema ili kupata mlo bora unapotoka kazini siku ya ijumaa jioni. Mishumaa, maua, matandiko mazuri ya meza, na vyakula bora vinaweza kuweka sabato kuwa spesheli kwa familia. Familia yako watafurahia utamaduni ya kibinafsi unaofanya abato kuwa spesheli.

Wakristo wetu wamepata uhuru mpya na furaha kubwa kwa kuishika sabato. Usiku ya ijumaa inakaribishwa kama wakati wa kuwa na familia, kufurahia chakula cha jioni, na kusoma maandiko mengine. Jumamosi huleta nafasi ya kulala, kushiriki kama familia, kusoma, na kuweka wakati wa maombi na kutafakari.

Kwa uhuru wa kufurahia sabato, ni sawa kushangaa juu ya kile kinachoweza na kisichoweza kufanywa wakati huu. Kuna hali ambazo zinawahitaji washirika kuamua kile Mungu atataka wafanye siku ya sabato. Utofauti wa kutazama sabato (k.v wengine wanaweza kuchagua kwenda katika hoteli, na wengine hawatafanya hivyo) sio msimamo wa kutoshiriki na wengine. Kanisa haiweki vitu vya kufanya na kutofanya kwa mapumziko ya sabato ila ya kusisitiza kanuni za kibiblia na mfano wake Yesu. Maandiko mengi ambazo zinazingatia sabato, haya mbili zinatoa ufahamu wa ibada na shughuli za sabato:

1. Marko 2:27-28: *"...Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato: Basi mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato pia."*
2. Isaya 58:13-14*: "Kama ukigeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu yangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku*

*takatifu ya BWANA, yenye heshima; ukiitukuza kwa kutozifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta ya kupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika BWANA; name nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka…"*

## Elimu kwa Vijana

Kanisa la Mungu la Kimataifa linatoa huduma za elimu kwa vijana. Ndizo hizi:

- Shule ya sabato: Iwe ni kwa kanisa au katika ushirika, vijana wanaweza kushiriki katika shule ya sabato. Ikiwa kuna vijana wa kutosha katika kusanyiko, elimu wa kiumri inahimizwa. Na ufahamu vizuri, vijana wanapewa madarasa kujifunza kuhusu Mungu na Biblia. Kusanyiko hupanga shule yao sabato kulingana na ratiba ya wakurugenzi, wazazi na vijana.
- INFUSE: Hii mpango wa kila mwaka inaelekezwa kimsingi kwa vijana. Inahusisha gazeti ya mtandao inyochapishwa baada ya kila mwezi tatu. Inaweza kupatikana katika tovuti ya kanisa: www.cgi.org Makala zinajadili mada zilizo muhimu kwa maisha ya vijana. INFUSE pia ina mpangilio wa huduma za kanisa kwa vijana kwa sehemu zilizotengwa kwa kusherehekea Sherehe ya Hema. Ikiangaliwa na huduma ya kikanisa, sehemu hizi zinatoa ibada (nyimbo, mahubiri, masomo za kibiblia, majadiliano) na shughuli zilizoundwa kwa matumizi ya kanisa. INFUSE pia husimamia ushirika na kutoa malengo. INFUSE ni njia ya ajabu kwa vijana kufanya kazi na kuhudumu pamoja.

Ingawa kila ya hizi mipangilio zimeundwa kwa umri maalum, vijana wanaweza kuhusika katika mipangilio kadhaa kwa wakati.

## Sherehe za Mwaka

Kwa sasa pengine unajua kwamba Kanisa la Mungu la Kimataifa haitazami mengi za sikukuu za kitamaduni. Unaweza kutafuta Biblia yako na ukose kupata wakristo wakipita krismasi, pasaka, sherehe za kichawi, na kadhalika. Sherehe za kibiblia

(au “nyakati zilizotengwa”) vimehusishwa na mavuno za kila mwaka za Israeli ya kale, moja majira wa chemchemi (mavuno madogo) na kimoja kwa majira ya majani kupukutika (mavuno makubwa zaidi). Msimu hizi za mavuno ni ukumbusho wa baraka za Mungu na mpango wake inayoashiria mavuno ya wafuasi (Yohana 4:35-38).

Orodha halisi ya sherehe za Mungu kila mwaka inapatikana kwa Mambo ya Walawi 23. Kwa sababu maarifa hii ni kipya kwa watu wengi sana na sio kawaida kwa kile ambacho Biblia kinafunua, tafadhali soma mwongozo inayotoa jina la sikukuu na maandiko yanayounga mkono utazamaji wake katika Agano la Kale na Agano katika Jipya. Zinajulikana kama:

| Sherehe | Agano la kale | Agano Jipya |
|---|---|---|
| Pasaka | Mambo ya Walawi 23:5 | Mathayo 26:2, 17-19<br>Marko 14:12-16<br>Luka 2:41-42; 22:17-20<br>Yohana 2:13,23; 6:4; 13:1-30<br>1 Wakorintho 11:23-29 |
| Mkate usiotiwa Chachu | Mambo ya Walawi 23:6-8 | Mathayo 26:17<br>Marko 14:12<br>Luka 2:41-42; 22:1,7<br>Matendo 2:3-4; 20:6<br>1 Wakorintho 5:6-8 |
| Siku ya Pentekoste | Mambo ya Walawi 23:15-22 | Matendo 2:1-21; 20:16<br>1 Wakorintho 16:8 |
| Siku ya Kuzipiga Baragumu | Mambo ya Walawi 23:23-25 | Mathayo 24:30-31<br>1 Wathesalonike 4:16-17<br>Ufunuo 11:15 |
| Siku ya Upatanisho | Mambo ya Walawi 23:26-32 | Matendo 27:9 |
| Sikukuu ya Vibanda | Mambo ya Walawi 23:33-43 | Yohana 7:1-2,8,10,14<br>Matendo 18:21 |
| Kusanyiko Takatifu | Mambo ya Walawi 23:36 | Yohana 7:37-38 |

Sherehe hizi kwa wazi zinatambuliwa kama “Sikukuu za Bwana” (Mambo ya Walawi 23:4, 37). Zilitazamwa na Israeli ya kale (Agano la Kale) na pia Mitume wa kwanza na wanafunzi (Agano Jipya). Ni muhimu kwamba sherehe hizi hatimaye zitatazamwa na kila mtu (Zekaria 14:16). (Andika kwa kijitabu bila ya malipo juu ya Mpango wa Mungu kwa maelezo zaidi kuhusu sikukuu kila mwaka.)

Kwa sababu Sikukuu za kila mwaka zina amuliwa kupitia kalenda ya lunar, hazifiki katika siku sawa au wakati mwingine hata kwa mwezi ile moja kila mwaka. Ile kusaidia kusuluhisha uwezekano wa kuchanganyikiwa juu ya siku ambazo sherehe hizi zinapaswa kutazamwa, kanisa huchapisha kalenda ya sherehe hizi inayoorodhesha sherehe za kila mwaka kulingana na kalenda ya kirumi.

Wakati mwingine watu wazima, huomba ruhusa kutoka kwa waajiri wao ili kutazama hizi sikukuu, wanaombwa “kutoa ushahidi” wa ombi lao. Hii ni sawa kwa wale walio shuleni. Wakati ombi hilo linahitajika, barua ya maelezo inaweza kutolewa na mtumishi au katika ofisi yetu ya kinyumbani kule Tyler. Kwa ukweli, ni vizuri kujulisha mapema mwajiri, mwalimu au shule.

Kutazama sherehe za Mungu ni ukumbusho kwa kile Mungu anahitaji kwa ubinadamu… lile sababu na chanzo cha wanadamu kuumbwa. Sherehe hizi zinatuelekeza kwa mwokozi wetu, Yesu Kristo. Sherehe ya kwanza inaonyesha Yesu kama mkombozi wetu. Kwa kuchukua katika Kristo – *mkate usiotiwa chachu* wa maisha – tunaweka dhambi kando. Kristo ndiye aliyekuwa matunda ya kwanza, na ilikuwa kupitia ufufuo wake Roho Mtakatifu ukatolewa kwa mwanadamu – *pentekoste.* Kristo ataingilia kati katika mambo ya ulimwengu Siku ya kuzipiga *baragumu* na kuwa Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Shetani, mpotevu mkubwa wa ubinadamu, atafungwa na kuzuiliwa. Wale waliompokea Kristo watakuwa naye kupitia toba, batiso, na kukaa katika maeneo ya Roho Mtakatifu, wakisamehewa dhambi zao – na *Kupatanishwa.* Kristo ataunda serikali yake na kuiongoza ulimwengu huu. Sisi sasa ni “wajumbe” wa ufalme huo tunapoishi katika mafunzo ya Yesu – *Sikukuu ya vibanda.* Mwishowe, wokovu itakuwa kwa kila mtu ambaye hajawahi kupata nafasi ya kujifunza njia za Kristo – *Kusanyiko Takatifu.*

Unapojitahidi kupitia mwaka na kutazama sherehe, utajifundisha kila sherehe na maana yake. Maana mingine huingiliana au huweza kufananishwa katika sherehe

zaidi ya moja. Unapoelewa maana ya siku hizi, mpango wa Mungu kwa binadamu itaanza kujifunua.

## Sheria za Lishe

Kanisa la Kristo la Kimataifa hutazama sheria za lishe ambazo Mungu aliwapa watu wake, jinsi ilivyorekodiwa katika Mambo ya Walawi 11 na Kumbukumbu la Torati 14. Sura hizi zinaeleza wanyama "utakaokula" na zile ambazo hutapaswa kukula kwa sababu ni "machafu." Kati ya nyama isiyo safi ni nguruwe, furokombe, kipungu, kengewa, na kozi.

Swali juu ya mahitaji ya Agano Jipya kuhusu wakristo kutazama sheria hizi za lishe imajadiliwa sana kwa miongo mingi. Hoja dhidi ya utazamaji wa sheria hizi zimo katika vikundi viwili – Ni za "kiyahudi" au "zimetupuliwa mbali." Kanisa la Mungu la Kimataifa haikubaliani na misimamo hizi. Hakuna ushahidi kuwa Mungu alitoa sheria hizi nje ya upendeleo wa kikabila; wala hakuna mifano katika Agano Jipya inayoruhusu ulaji wa nyama isiyo safi. Hata hivyo tunaweza kuuliza kwa nini Mungu alimpa mwanadamu sheria hizi (kwa afya yao?), sababu inayotolewa katika Mambo ya Walawi 11:44 inatosha: "Kwa kuwa mimi ni Bwana, Mungu wenu; takasane nafsi zenu basi; iweni watakatifu, kwa kuwa mimi ni mtakatifu…" kifungu cha 47 inaiweka wazi kabisa kwamba Mungu, yule aliyewaumba wanyama wote inaeleza "tofauti kati ya chafu na safi, na kati ya wanyama wanaoweza kulwa na zisizoweza kulwa." (Ukitaka maelezo zaidi juu ya sheria hizi za lishe, tafadhali wasiliana na mmoja wa watumishi wetu au utuandikie kwa maelezo zaidi.)

## Sadaka na Zaka

Sadaka na zaka ni maonyesho ya kibinafsi za ibada. Jinsi mtu anavyotoa ni juu yake. Hakuna mapokeo (za kifedha) kutoka kwa kusanyiko la sabato kila wiki. Hata hivyo, kwa kuwa kuna sherehe zilizoamuriwa na kuhusiana na utazamaji wa sheria kila mwaka (Kumbukumbu la Torati 16:16), sadaka zinapokolewa siku hizi kuu katika mwaka. Sadaka na zaka za kawaida huwa zinatumwa katika ofisi ya kinyumbani kule Tyler.

## Habari za Kanisa na Maelezo ya Huduma

Kujulisha kila mkristo kuhusu tukio za kanisa ni mgumu sana. Chanzo cha msingi ya habari kuhusu kanisa ni habari ya kimataifa, barua za kila mwezi, na tovuti ya kanisa. Ili kuhakikisha unapokea chapisho zetu kila mwezi unapaswa kuwa katika orodha yetu kupitia anwani yako. Ujumbe moja muhimu: Ikiwa program za tarakilishi zetu hazioni shughuli katika rekodi yako (ombi la fasihi au usaidizi likitumwa) kwa miezi sita, itawacha kutuma kwa anwani yako. Utaratibu huu ni muhimu kwa kuharibu fedha kwa kutuma kwa wale ambao wamehama au hawahisi kutumiwa tena. Kama unafikiria umekosa kupokea kutoka kwetu (na unataka utumiwe), tuandikie au tupigie ili kurekebisha ombi lako.

Chanzo kingine muhimu ya habari ni kazi za Kanisa la Mungu la Kimataifa. Hili sasisha kila wiki limo kupitia ombi kwenye mtandao. Huduma hii hutoa habari za takwimu (majibu kupitia runinga, mapato) pia na ombi la ushirika, ziara za watumishi zinapokuja, na tangazo maalum. Ikiwa ungetaka kupata huduma zetu tafadhali tujulishe.

Raslimali nyingine ya "kuwasiliana" ni huduma ya kikanisa kupitia tovuti. Ili kupata kusanyiko hizo zikituma huduma zao za sabato, nenda kwa tovuti ya Kanisa la Kristo la Kimataifa (www.cgi.org) kisha ubonyeze *live webcasts*. Ikiwa unayo tarakalishi inayoweza kuhifadhi video na uwezekano wa upesi wa kimtandao, basi unao uwezo wa kutazama mahubiri. Hii inatolewa kama huduma kwa wale wasioweza kuwa katika kusanyiko na haipaswi kuchukua mahali pa sabato "wala tisiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi ya wengine.

## Elimu na Mafunzo

Kanisa la Mungu la Kimataifa inahimiza kusanyiko za mtaani kuanzisha mafunzo za ukomavu wa kibinafsi kwa wafwasi wao. Hii inaweza kuwa katika njia ya mafunzo za hotuba, masomo ya kibiblia, maendeleo ya kibinafsi, ukomavu wa kikristo, kuongoza nyimbo, na mafunzo ya uongozi. Wale wanaofundisha program wanapaswa kuwa na usaidizi wa mtumishi aliyedhaminiwa na kupokelewa vizuri na wale wanaohitaji elimu na mafunzo. Mafunzo za programu zinapaswa kuwa na malengo na kuundwa kwa matokeo iliyo na mpangilio.

Wanafunzi kwa kazi ya utumishi wanapaswa kuhusishwa katika usaidizi kwa utumishi. Programu hii inatambua na kuendeleza "zawadi" ya utumishi. Wale wanaoshiriki watakuwa na faida ya kujishuhudia wenyewe kupitia masomo, tathmini, na hotuba wa umati. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na mshauri atakaye simamia ukamilikaji wa changamoto za kimaandishi na hotuba. Ingawa kunaweza kuwa na marekebisho kila mara kwa urefu wa programu, ushiriki huchukua mwaka moja hadi tatu. Hii huhalalisha sifa kwa uwekaji na kazi uchungaji.

## Kanuni ya Wazi ya Kanisa

Kanisa la Mungu la Kimataifa ni kanisa wazi. Kunao watu wanaotutembelea walio wapya katika imani. Wengine hawawezi kuzishika sheria za Mungu jinsi wanavyopaswa, na wengine hawana imani kwa kila kitu tunayofunza. Tunaomba waweze kuhimizwa kupitia huduma tunazotoa na kuweza kutembea karibu na Mungu. Tunaomba usihukumu au kuweka kiwango chako cha utiifu kulingana na kile unachomwona ndugu yako akifanya. Kristo ndiye kiwango chetu, sio watu wadhaifu wenye dhambi. Kumbuka kila mara kwamba utahukumiwa kwa kile unachofanya, sio kile wengine wanafanya. Kazi yako ni kuwaombea na kumfurahisha Mungu kwa kila kitu unachofanya.

*Yeye aliye dhaifu wa imani, mkaribisheni, walakini msimhukumu mawazo yake. Mtu mmoja anayo imani, anakula vyote; lakini yeye aliye dhaifu hula mboga. Yeye alaye asimdharau huyo asiyekula, wala yeye asiyekula asimhukumu huyo alaye; kwa maana Mungu amemkubali. Wewe u nani unayemhukumu mtumishi wa mwingine? Kwa bwana wake mwenyewe yeye husimama au huanguka. Naam, atasimamishwa kwa kuwa Bwana aweza kumsimamisha (Warumi 14:1-4).*

## Maombi kwa wengine

Ni mazoea ya huduma ya ofisi ya kinyumbani kuwaombea wale wanaowasiliana na sisi na maombi yao. Hii hufanywa kila wiki au kulingana na hali inavyotokea. Iwapo unakuwa mgonjwa, au kuna ugonjwa kwa familia yako, au wakati mgumu usiowezana nayo, au msiba unaohitaji maombolezi, au mahitaji yoyote ya

maombi… tuandikie, tupigie simu au tutumie barua pepe ili kutujulisha. Maombi zote zinasomwa na kuinuliwa juu kwa Mungu. Tunakuja kwa Mungu ili kuingilia kati, tukimwomba kujibu kwa imani ya wale waliohusishwa. Tunatilia maanani tukijua kwamba *"kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana"* (Yakobo 5:16)

## Uongozi

Uongozi wa Kanisa la Mungu inamilikiwa na huduma. Kanisa la Mungu la Kimataifa ni ushirikiano wa Texas, ikiongozwa na baraza la wakurugenzi. Baraza hili limeteua mambo yote ya huduma kwa kundi linalowashauri wakuu wa kanisa, na kutoa mwelekeo kwa makanisa madogo, kuwaweka watumishi na kuzisikiliza matatizo yanayohusiana na huduma.

Mafunzo ya kanisa yamewekwa katika Kauli zetu za Imani na ziko imara. Mabadiliko kwa mafunzo ni nadra na haikuji kupitia uongozi wa juu bali kwa majadiliano na maagano wa huduma.

Tunachapisha Mwongozo kwa Makanisa madogo kuorodhesha kanuni na maelekezo kwa makanisa. Zinaondolewa kama maelekezo zilizoko na viwango vya kutiliwa maanani baadala ya "maandishi yalioandikwa kwenye kidonge cha jiwe."  Kupitia tukio za hali maalum, nakali hii hurekebishwa kila mara ili kufikia matarajio ya kanisa linalokuwa. Maoni zote muhimu kutoka kwa mwongozo huletwa kwa wakubwa ili kuzingatiwa.

Kusanyiko na vikundi vya ushirika vinavyotambuliwa na Kanisa la Mungu la Kimataifa hufanya pamoja kwa kuihubiri injili na kutoa "hekalu" kwa ibada ya kijumla.

Kusanyiko zetu mingi ziko huru, lakini zinapoendelea, wao kupitia umuhimu huwa na utaratibu. Jinsi Paulo alivyosema, *"vitu vyote na vifanywe kwa utaratibu."*

Msingi wa vyote tufanyayo ni sheria ya Mungu, lakini hakuna kanuni za kisheria zilizoweza kuandikwa kusimamia uwezekano wa kila tendo la kibinadamu. Hata katika maisha ya Musa, hali zilitokea zisizosimamiwa na amri na sheria. Kwa hivyo, Musa alimwuliza Mungu kile cha kufanya, na kikundi cha tatu cha sheria ziliwekwa ziitwazo "hukumu." Kwa kuongezea hukumu za Mungu, aliweka

waamuzi kuamua mambo mazito na kuweka amri nyuma ya hukumu zao jinsi alivyojiwekea (Kumbukumbu la Torati 17:8-13).

Katika Agano Jipya, amri sawa ilipewa kwa huduma (Mathayo 16:19; 18:18; Yohana 20:23). Hii sio amri ya kubadilisha sheria za Mungu, lakiniya kutoa hukumu jinsi ya kuitii sheria. Hukumu za kanisa zilizoongeka kwa wakati uliunda tamaduni za kanisa. Kwa hivyo tukisema kuwa kitu ni tamaduni ya kanisa, tunamaanisha kwamba hii ni hukumu (kulingana na habari iliyoko wakati huo) kwa kile ambacho Mungu anatuhitaji kufanya kama kanisa.

## Ubatizo na Ushirika

Kupitia mifano ya kibiblia na mafunzo, tunajifunza kuhusu ubatizo. Paulo kwa mfano alilinganisha ubatizo kama "kuzikwa naye [Kristo] katika kifo." Kristo, akizichukua dhambi za wanadamu, alizikwa kwa kaburi ya kimwili; sisi tukiwa na dhambi zetu tunazikwa (kuzamishwa) katika kaburi ya maji. Basi, Kristo alipofufuka kutoka kaburini katika maisha mapya, sisi pia tunafufuliwa kutoka kwa kaburi ya maji kama "viumbe vipya" (2 Wakorintho 5:17). Dhambi zetu zinazikwa na kusamehewa; "vitu vyote vinakuwa vipya."

Haja ya ubatizo huja kupitia kujielewa kibinafsi, imani, kisha toba. Tunajiona kama wanadamu wasio kamilifu ambao watenda dhambi kwa sheria za Mungu. Tunajuta kwa dhati kukataa kwetu wa njia zake. Tunasema pole kwa makosa zote tumefanya. Tunatubu. Tunatoka kwa njia zetu za dhambi na kuomba msamaha wa Mungu.

Maswali mawili yanaulizwa kwa yule atakaye kubatizwa:

1. Umetubu dhambi zako, ya kutotii amri za Mungu zilizo takatifu na za haki?
2. Unakubali Yesu Kristo kama mwokozi wako wa kibinafsi?

Jibu la uhakika kutoka moyoni ndicho kinachohitajika kwa ubatizo. Baada ya ubatizo ni sherehe ya kuwekewa mikono kwa upokeaji wa Roho Mtakatifu (Matendo 8:16-18). Kwa kufuata mifano ya mitume, mikono yanawekelewa kichwani mwa yule aliyebatizwa na maombi kufanywa ili kumwomba Mungu kumtumia mtu yule Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu haitambuliki kupitia hisia,

kwa hivyo hakuna matarajio ya maonyesho ya kiroho. (Tukio yanaotolewa katika sura ya pili ya Matendo ni za kipekee.)

Tunabatiza wapi? Washirika wamebatizwa katika mito, ziwa, mabwawa, chombo cha kuoga, tangi za ubatizo, na, katika sehemu inayokuja akilini, mtumbwi uliojazwa kwa maji. Maji yapaswa kuwa ya kutosha kwa uwezekano wa kuzamishwa.

Unapaswa kuwa wa umri gani unapobatizwa? Wakati Biblia haisemi umri maalum inatoa mifano ya kutafakari ufahamu na uwajibikaji. Hitimisho dhahiri ni kuwa mtu anapaswa kubatizwa ikiwa ako tayari – wakati anaelewa kile ambacho ni dhambi na matokea ya matendo zake.

Tunavaa nini tunapobatizwa? Nguo rasmi "zisizoonekana kupitia"

## Kubatizwa Tena

Sio kawaida kuwa tunaulizwa ikiwa inahitajika kwa mtu aliyekuwa amebatizwa "kubatizwa tena." Ingawa maandiko yanatoa mfano wa kibiblia ya sherehe kama hizo, haihitajiki. Katika Matendo 19:1-6, kuna tukio ya wafuasi wengine kule Efeso. Paulo alipokutana nao, aliwauliza, "mmepokea Roho Mtakatifu tangu msadiki?" Ni muhimu kuelewa kwamba njia moja tu Paulo alileta ilikuwa ikiwa walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu. Haikujalisha nani aliwabatiza. Kile Paulo alitaka kujua ilikuwa ikiwa matunda ya Roho Mtakatifu yalionyeshwa kwa maisha yao tangu ubatiso.

Katika kesi hii, watu hawakujuwa chochote kuhusu Roho Mtakatifu. Paulo alipowauliza, "basi mlibatizwa kwa ubatiso gani?" Wakasema kwa ubatizo wa Yohana, ambayo ilikuwa batiso ya toba. Paulo alipowaelezea kila kitu, walibatizwa tena, na kupokea kuwekelewa mikono kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

Jambo moja la ilani: Wakati mwingine mtu anihisi kuwa anapaswa kubatizwa tena kwa sababu hakukuwa na maonyesho ya Roho Mtakatifu. Paulo anatuambia kuwa matunda ya Roho Mtakatifu ni upendo, furaha, amani, uvumulivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi (Wagalatia 5:22). Hizi ndizo matunda unayopaswa kutafuta unapoamua ikiwa ubatiso wa kwanza ulikuwa halisi. Pia kumbuka ahadi

ya Mungu. Ikiwa umefanya toba na kubatizwa kwa Jina la Kristo, basi una *ahadi* ya Roho Mtakatifu.

Wakati mwingine mtu anataka kubatizwa tena kwa sababu amefanya toba sana tangu batizo ya kwanza. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Toba ya kindani ni ushahidi wa Roho Mtakatifu katika maisha yako. Haimanishi unapaswa kubatizwa tena.

Uamuzi wa mwisho kuhusu kubatizwa tena ni wa mtu anayehusika. Uamuzi huo unapaswa kuchukuliwa kwa maombi, na ushauri, ikihitajika. Ikiwa mtu anahisi hakufanya toba baada ya ubatizo, na kuwa matunda ya Roho haimo katika maisha yake, basi kunaweza kuwa na uwezekano kwa kubatizwa tena. Ikiwa mtu alifanya toba kabla ya ubatizo ya kwanza na ameweza kupotea, kubatizwa tena sio lazima. Kufanya toba upya na kujitolea tena kwa Mungu inafaa kubadilisha maisha yake.

## Hitimisho

Jinsi unavyoweza kuona kwa kile ambacho umesoma, Kanisa la Mungu la Kimataifa ni familia ya wafuasi sawa wanataka kuhusisha badala ya kutohusisha. Sisi ni sehemu ya mwili wa Kristo. Watu wanaokuja kwetu kwa usaidizi hawahitajiki kuwa wakamilifu kabla ya kuja kwa kanisa. Wanajiunga nasi kwa kuhimizwa na kuelewa, na pia nafasi ya kupata habari njema kuhusu kuishi kwa hii dunia ili kuweza kuishi katika ile ijayo.

Ni kawaida ya Kanisa la Mungu la kimataifa kuwa hatuhitajiki kuwatawala washiriki wetu. Tunataka kuhudumiana kupitia zawadi za kiasili na za kiroho. Kwa ukosefu wa ndoano ya kiroho (k.v, “sisi ni kanisa pekee,” “sisi ni Philadelphians,” “sisi ni kanisa la kweli la Mungu,” “sisi ni spesheli,” n.k.), ufuasi wetu umeundwa baada ya uongozi wa kitume. Yesu, baada ya kuuliza, “ni nani basi aliye wakili mwaminifu mwenye busara?” alijibu, “heri mtumwa yule ambaye bwana wake ajapo atamkuta anafanya hivyo” (Luka 12:42-43). Tunaweza kufanya vizuri kwa kuhudumia wanadamu wenzetu. Ukihisi hivyo utapata burudisho katika Kanisa la Mungu la Kimataifa.

Ili kufafanua Paulo 2 Timotheo 4:6-8, tunaomba kwamba utavipiga vita vilivyo vizuri, kumaliza kile ulichoanzisha na kuilinda imani ili kuwekelewa taji ya haki.

Asante kwa kuchukua mda wa kujifunza kuhusu kanisa letu na tamaduni zetu za ibada. Karibu kwa familia yetu! Mungu akubariki na kukuleta kwa ufalme Wake. Ni upendeleo wetu wa kukusaidia hadi hapo.